USAHIHI WA SALA YA MAITI
NA
YALE YANAYOFUNGAMANA NAYO
KWA MUJIBU
WA
KITABU NA SUNNA

KIMEANDALIWA
NA
ABUU MUHAMMAD
HASNUU AMOUR KOMBO

Markazil-Farouk
Zanzibar

UTANGULIZI

Kila sifa njema anastahiki Muumba wa kila kitu ambaye amemtuma Mtume wake kuwa ni rehma kwa kila atakaemfuata Mtume huyo.
Ama baada ya hayo tumeonelea kuweka kijitabu cha sala ya maiti ili kuwasaidia waislamu katika kuitekeleza dini katika usahihi wake.

Allah afanye wepesi na atie tawfiq

Amin

Markazil-Farouk
Zanzibar

SALA YA MAITI NA NAMNA YA KUMSALIA MAITI KWA MUJIBU WA MAFUNDISHO YA MTUME (SALALLAHU ‘ALAYHI WASALLAM)

Sala ya maiti ni faradhi kifaya kwa maana wakiitekeleza baadhi ya waislamu waliyobaki ambao hawajaitekeleza jukumu, wajibu na dhimma imekwisha ondoka na ikiwa hakuna katika waislamu waliyoitekeleza sala hiyo basi jukumu, wajibu na dhimma itakua ipo na itakua juu ya kila muislamu.

Sala ya maiti ni sala ambayo haina rukuu wala sijida na ina takbira {4} na zipo riwaya zinazoonyesha kuwa inaruhusika takbira tano {5} mpaka takbira {9}, yote hayo yamethibiti kutoka kwa Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam} na sala hiyo ni wajibu kusaliwa kwa jamaa kwani hajapatapo kuonekana Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam} kuisali sala hiyo peke yake pasi na jamaa na maswahaba zake juu yao radhi kutoka kwa ALLAH ziwafikie.

Inajuzu sala ya maiti kusaliwa ndani ya msikiti kwa hadithi ya Bi Aisha Radhi za ALLAH ziwe juu yake, ambayo ameitoa hadithi hiyo Imam Muslim {Angalia Muslim 3/63} na {Sunanil-bayhaqiyyu 4/51} lakini lilokua bora zaidi ni kusaliwa nje ya msikiti kama lilivyokua jambo hilo katika zama za Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam} {Angalia hayo katika Bukhari {3/155}, Sunanil Ahmad {5/289}, Mustadrakil-Hakim {2/24}, Targhiybul-Muudhiyyi {3/34}.

Imamu atakayesalisha sala ya jeneza anatakikana asimame nyuma ya kichwa cha yule maiti ikiwa huyo ni mwanamme na atatakikana asimame katikati ya maiti ikiwa maiti huyo ni mwanamke kama lilivyothibiti jambo hilo katika sunna kutokana na hadithi iliyopokelewa na Abuu Ghalibu Khayyatwi ambaye ameitoa hadithi hiyo Imamu Abuu Daudi, Imamu Tirmidhiyyu, Ibnu Maajah, na Twahawiy, na Bayhaqiyyu na Twayalisiyyu na Imamu Ahmad {Angalia Sunanil-Bayhaqiyyu {4/32}, Musnad Ahmad {3/118, 204}.

NAMNA YA KUSALI

Tia nia yako ya kusali sala ya maiti ambayo nia hiyo pahala pake ni moyoni ama jambo la kutamka matamshi si katika jambo la sunna bali ni uzushi uliozuliwa, baada ya kutia nia yako hiyo soma takbira ya mwanzo na baada ya takbira hiyo soma suratul-fatiha na sura nyengine, jambo hili limethibiti kwa Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam} kutokana na hadithi ya Ibnu ‘Abbasi ambayo ameitoa imamu Bukhary, Abuu Daud, Annasai Tir-midhiyyu, Ibnu Jarudi, Addaraqutwiniyyu na Imamu Hakim {Angalia Bukhary {3/158}, Sunani Abuu Daud {2/68}, Sunani Annasai {1/281}, Sunani Tir-midhiyyi {2/142}, Al-muntaqaa {264}, Sunani Addaraqutwiniy {191}, Mustadraq {1/358-386}.

Baada ya kumaliza kusoma Suratul-Fatiha na sura nyengine, soma takbira ya pili baada ya kutamka takbira ya pili msalie Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam} kwa kusema hivi ifuatavyo:-

اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيْمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيْمَ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيْمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيْمَ، فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيْدٌ مَجِيْدٌ.

Kisha unasoma na kutamka takbira ya tatu baada ya kutamka takbira hiyo soma dua kumuombea maiti Nayo ni hii ifuatayo:-

اللّٰهُمَّ عَبْدُكَ وابْنُ أَمَتِكَ, احْتَاجَ إِلَى رَحْمَتِكَ, وَأَنْتَ غَنِيٌّ عَنْ عَذَابِهِ، إِنْ كَانَ مُحْسِنًا فَزِدْ فِي حَسَنَاتِهِ، وَإِنْ كَانَ مُسِيْئًا فَتَجَاوَزْ عَنْهُ.

TANBIHI: Dua za kumuombea maiti zimekuja katika sunna aina nyingi ambazo zimethibiti kwa Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam}, kwa hiyo ni juu ya Muislamu kuhuwisha mwenendo wa Mtume {Salallahu ‘alayhi

wasallam} kuzifanyia kazi aina hizo, lakini sisi tumeichagua dua hii tulioiandika hapa juu kwasababu ni nyepesi kuhifadhiwa kutokana na ufupi wake.

Kisha baada ya kutamka takbira ya tatu na kuomba dua hiyo utasoma na kutamka takbira ya nne na utamuombea maiti dua hiyo au nyengine katika zile aina zilizothibiti kwa Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam}, na jambo hili la kumuombea dua maiti katika takbira ya nne limethibiti vile vile {Angalia Sunanil-Bayhaqiy 3-35, 4/42, 43}, Sunani Ibnu Maajah {1/457}, Mustadrakil-Hakim {1/360}, Musnad Ahmad {4/383} na pia angalia Kitabul-Janaaiz cha Shekh Albaniy na Sherehe Mumtii cha Shekh Ibnu Uthaymin.

Ukimaliza Takbira ya nne na dua ya kumuombea maiti utatoa salamu na utakua umemaliza kumsalia maiti, kwa sala inayojuulikana kwa jina la sala ya maiti.

FAIDA ZA KIELIMU

1) Katika takbira ya mwanzo yaani takbira ya kuhirimia sala unaruhusika kunyanyua mikono lakini takbira zinazofuata hapajathibiti kutoka kwa Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam} jambo la kunyanyua mikono katika takbira zilizobakia.

2) Ikiwa patasaliwa maiti kwa sala yenye takbira zaidi ya nne basi katika hizo za ziada ataombewa dua maiti mpaka kumalizika kwa sala hiyo.

3) Kwa mfano maiti ni wengi sana Je! Tunaweza kuwakusanya na kuwasalia sala moja tu? **JAWABU**: Naam tunaweza kuwakusanya na kuwasalia sala moja kwa wote, na maiti za kiume zitawekwa upande anaofuata imamu kisha zitafuata maiti za kike. Jambo hili limethibiti katika sunna kutokana na hadithi ya Naafii kutoka kwa Abdillah bin Omar ambayo ameitoa hadithi hiyo Imam Annasai {1/280} Ibnu

Jaruudi katika kitabu chake Al-muntaqaa ukurasa {267} na {268} na Addaraqutwiniy ukurasa {194} na Al-Bayhaqiy katika sunani yake {4/33} na ameisahihisha Sheikh Albaniy.

4) Baada ya kusaliwa sala ya maiti hakuna dua wala uradi na wala Ikh-laswi ngapi someni, hamna mambo haya kwa maana hayajathibiti kutoka kwa Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam} na atakaefanya haya atakua amekwenda kinyume na sunna, kinachotakikana baada ya kumaliza sala ya maiti ni kuchukuliwa jeneza na watu kuelekea makaburini kwa ajili ya kumzika mwenzao kwani ile sala iliyosaliwa ndio dua yenyewe aliyoombewa maiti sio watu kuzusha mambo kwenye dini, na sisi hapa tunatoa chalenji hakuna dalili juu ya jambo hili na kama ipo, ipo wapi na ipo vipi?!

5) Baadhi ya ndugu zetu wanapotoa salamu ya kumalizia sala ya maiti huengeza neno nalo ni:-
{ASSALAM ALAYKUM WARAHMATULLAHI TA’ALA WABARAKATUH}
Kwanza tamko **“TA’ALA”** halijathibiti katika Sunna bali kulitamka tamko hili mahala hapa ni uzushi huenda mtu akauliza kwani nini maana ya **“TA’ALA”**?
JAWABU: Hapazingatiwi maana ya kitu wala faida ya kitu kwanza huzingatiwa kuthibiti kwa kitu hicho kisha ndio tena hapa huangaliwa maana na faida inayopatikana katika kitu hicho.
Pili, tamko **“WABARAKATUH”** tamko hili baadhi ya ndugu zetu wamelifanya ni katika salamu inayotolewa katika sala ya maiti tu na ilhali tamko hilo limethibiti katika sala za kawaida vile vile tena limethibiti upande wa kulia tu pasi na kutolewa upande wa kushoto bali upande wa kushoto utatoa salamu pasi na kulitaja tamko hilo, dalili ya hayo ni hadithi iliyosimuliwa na Wayli Ibni Hujri hadithi ambayo ameitoa Imam Abuu Daud katika sunani yake nambari ya hadithi hiyo ni {997}, na ameisahihisha Imamu Al-baniy na wengineo.

6) Zinapokusanyika sala ya faradhi na sala ya maiti hutangulizwa sala ya faradhi kisha ndo husaliwa sala ya maiti, lakini watu wengi hivi sasa hatufatilii mambo ya dini yetu hujifanyia mambo bila ya elimu sahihi kutoka kwa Mtume {Salallahu ‘alayhi wasallam} kwa ufahamu wa wale wema waliotangulia, Masahaba, Matabiina na Matabi tabiina na waliyowafuata hao kwa wema.

7) Wamekwenda baadhi ya Maulamaa {Wanazuoni} ya kwamba baada ya kutamka takbira ya nne ni kutoa salamu wala hakuna kusoma au kuomba dua katika takbira ya nne kuwa atasimama kidogo kwa maana baada ya takbira ya nne atasita kidogo kisha atatoa salamu, kuhusu kauli hii siyo sahihi bali ni kuomba dua kumuombea maiti. {Angalia hayo katika kitabu Al-Jamiul-Ahkaami Fiqhu Sunna {2/46} cha Shekh Ibnu Uthaymin na Ahkamul-Janaaiz cha Shekh Al-baniy.

8) Je! Katika sala ya maiti pameekewa sheria kusoma dua ya kufungulia sala?

JAWABU: Hapajaekewa sheria kusoma dua ya kufungulia sala, amesema Shekh Al-baniy katika kitabu cha Ahkamul-Janaaiz ukurasa {119} baada ya kueleza takbira ya mwanzo na dalili yake akasema “Ndani yake kuna ishara ya kukosekana kuekewa sheria jambo la kusoma dua ya kufungulia sala na huo ndio msimamo wa watu wa kishafi na wengineo na amesema Abuu Daudi katika “Masaaili {153}”.

والله أعلم

KIMETAYARISHWA NA KUANDIKWA NA

ABUU MUHAMMAD
HASNUU AMOUR KOMBO

Simu **+255776-819880**

Endelea kufuatilia nakala zetu za dini.